# UNAJUA KUWA MALALAMIKO NI MATOKEO YA WEMA ULIOPITILIZA?

**Na. Mwanawetu Mmuni**

**© 2022**

**Malalamiko** au kwa neno jingine manung'uniko; ni maelezo, maneno, au mazungumzo yanayotolewa na mtu asiyeridhika/kuridhishwa na jambo fulani alilofanyiwa au kutendewa na mtu mwingine, kikundi cha watu, taasisi, au serikali.

**Wema** ni mambo mazuri anayoyafanya mtu. Ni ari ya kumtendea mtu mema. Kwa maneno mengine katika lugha ya Kiswahili ni fadhila, fadhili, ukarimu, hisani, au jamala.

1. **Malalamiko yanayoweza kujitokeza katika kutatua kero za kisiasa**

Katika maisha halisi ya siasa, ukiwaona watu/wananchi wanalalamikia jambo au mambo fulani; tambua kuwa jamii hiyo imezoea kutendewa wema uliopitiliza hadi wamefikia hatua ya kuona wema huo ni jambo la

kawaida hivyo kusiwe na ukomo au wanadai kitu kingine cha ziada.

Haina maana jambo jipya wanalolilalamikia likitekelezwa wataacha kulalamika, la hasha! Watu hao wataweza kuendelea kulalamikia matokeo ya jambo lililofanyika. Mfano leo raia wanalalamikia kero ya maji. Kwa bahati nzuri maji yakapatikana, kesho watalalamikia kero ya nishati. Wakipata vyote pia hawatakaa kimya bali wataanza kulalamikia matokeo ya yale yaliyotekelezwa. Kama vile; kwenye maji wanaweza kuanza kulalamikia mgao wa maji, ikitatuliwa kero hiyo kwa kutoa maji masaa 24 mwezi mzima, watalalamikia ankara za maji kuwa ni kubwa hivyo wanashindwa kulipia. Ikitatuliwa kero ya ankra kwa kuboreshwa huduma za maji, watalalamika kuwa miongoni mwao kuna maskini wasioweza kujiunga na huduma hiyo wala kuwa na uwezo wa kulipa ankra za maji. Wakitatuliwa kero hiyo kwa kujengewa visima vya kuteka maji bure, wataacha watoto na mifugo wachezee maji na ikitokea mmoja wao akapata madhara pia watalalamikia kuwa maji ya bure yanawadhuru watoto wao au mifugo yao.

 *© 2022*

Hayo ndiyo malipo ya wema uliopitiliza yatolewayo na walalamishi kupitia siasa!

**SIASA → WEMA → MALALAMIKO HASIRA → MIGOGORO+VITA**

**Maoni**

*Shughuli za kisiasa;* kutatua changamoto/kero/matatizo ya wananchi ni vema kuzingatie sheria na taratibu za nchi, vipaumbele, au mipango-kazi ya kitaifa badala ya kutibu malalamiko.

## 2. Utatuzi wa changamoto za kifamilia

Malalamiko ya kifamilia yanayochangiwa na wema uliopitiliza yanaweza kujidhihirisha katika mambo yafuatayo;

*Uwajibikaji wa Mwanajamii au Mwanafamilia katika kutekeleza majukumu ya familia*. Majukumu; kusomesha watoto (kulipa karo za shule), kukidhi gharama za chakula na matibabu, mavazi, malazi, na mahitaji mengine.

Malalamiko kuwa ni matokeo ya wema uliopitiliza hujitokeza pia kwenye ngazi hii ya familia. Ipo hivi; kwenye ndoa, watu wengi wenye uhusiano unaopitia

migogoro/changamoto, mara nyingi ndoa zao hudumu kwa muda mrefu kuliko ndoa zenye utulivu.

**Sababu;** Mwenza anapopewa au kutekelezewa kila hitaji lake liwe la ari au mali, mara nyingi mtendewa huchukulia mazoea hali hiyo na kufanya jambo hilo kuwa la lazima. *Mfano* kupewa zawadi, kufanyiwa hisani, manunuzi makubwa kama gari, nyumba za kifahari, matembezi/kutalii, shamba, manunuzi ya nguo kwenye boutique, kusalimia ndugu na marafiki wa mwenza, mahaba, au mambo mengine.

Sasa ikitokea kitu kimoja kikapungua au kukosekana! Malalamiko yataanza na endapo hakutatokea jambo la kurudisha hali hiyo; mapenzi au uhusiano huweza kukoma ghafla kwa spidi ya kile kitu kimoja kilichokosekana. Wakati wale wenye mizozo mara kwa mara, hata ikitokea mke au mume kapigwa makonde na kutolewa ngeu! Hakuna malalamiko bali kutakuwa na kesi au usuluhishi wa tatizo lililotokea la ugomvi. Endapo watasuluhisha na kuombana msamaha kisha kutibiana majeraha, maisha yataendelea kama kawaida.

*Sababu* kwenye familia hii ya pili yenye migogoro inakuwa haina watu wenye kudai nyongeza ya mahitaji

ya msingi au wanaodeka. Kila mmoja anatekeleza mambo muhimu/ ya lazima na endapo ikitokea nyongeza basi ni nadra. Hivyo sio rahisi kwa mwenza kudhani jambo zuri/la wema alilotendewa ni wajibu au kitu cha lazima na kuanza kukidai au kukilalamikia pindi linapokosekana.

**Maoni**

Changamoto au matatizo ya kifamilia hayapaswi kuelezwa kwa njia ya malalamiko isipokuwa kwa kuelezana ukweli, kusikilizana, kukubaliana, kuthamini uwepo wa mwenza, busara, kufuata misingi ya mahusiano, kuzingatia miongozo ya mila na desturi za jamii, kuzingatia sheria za nchi, kuzingatia haki za binadamu, kuheshimiana, kufuata misingi ya dini, na kudumisha upendo badala ya chuki.

 *© 2022*